# JARIBIO LA NANE K.C.P.E
# DARASA LA NANE 2018

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Kande ni ya mawele kama ilivyo kicha kwa

A. barua
B. karata
C. funguo
D. noti

Jibu sahihi ni C

1 [A] [B] [C] [D]   11 [A] [B] [■] [D]   21 [A] [B] [C] [D]   31 [A] [B] [C] [D]   41 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa jawabu lifaal›› zaidi.*

Kuna aina mbalimbali ____1____ kila moja huwa na ____2____ muhimu inayotekeleza katika maisha ya mja. ____3____, elimu ya maisha hupatikana kutokana na ____4____ na wanajamii ____5____. Nyingine ni elimu ya vitabu ambayo ____6____ hupatikana katika shule na vyuo mbalimbali. Halikadhalika, ipo elimu ya dini inayomwezesha mtu kuishi kulingana na mapenzi ya Muumba wake. Sharti ieleweke kuwa ____7____ kujifunza mengi maishani. Elimu yoyote ile ____8____ kumwezesha mtu kuishi kwa uadilifu.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | ya elimu ambayo | za elimu ambayo | ya elimu ambazo | za elimu ambapo |
| **2.** | jukumu | dhima | lengo | kusudi |
| **3.** | Mathalani | Kwa hivyo | Hata hivyo | Aidha |
| **4.** | kutangamana | kutangatanga | kutengana | kutegemeana |
| **5.** | jingine | nyingine | wengine | zingine |
| **6.** | angalau | aghalabu | falau | muhali |
| **7.** | kadri tunayoendelea kukua ndiyo tunayoendelea | kadri tunapoendelea kukua ndipo tunapoendelea | kadri anayeendelea kukua ndiye anayeendelea | kadri tunavyoendelea kukua ndivyo tunavyoendelea |
| **8.** | ina budi | hapana budi | haina budi | pana budi |

Sarafina alikuwa na kipawa cha ____9____. Alikuwa mwimbaji mwenye sauti ya ____10____. Walimu wake walikitambua kipawa hicho ____11____ ajiendeleze. alianza kwa kuyaimba mashairi yenye mishororo minne katika kila ____12____; yaani ____13____. Baadaye alijiunga na kwaya ya shule ambapo kipawa chake ____14____ zaidi. Japo hakufanya vizuri katika masomo ya darasani, kipawa chake kilimfanya kuheshimiwa kote. Ama kweli ____15____

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | pekee | kipekee | dhati | adimu |
| **10.** | kurumbiza | kipanga | mwewe | njiwa |
| **11.** | wangemhimiza | wakimhimiza | walimhimiza | wakamhimiza |
| **12.** | kipande | aya | ubeti | ukwapi |
| **13.** | tathnia | tathlitha | robo | tarbia |
| **14.** | kulikulishwa | kulikuzwa | kililishwa | kilikuza |
| **15.** | Mguu mtembezi haukosi mwiba | Mtu huenda na uchao, haendi na uchwao | Kila chombo na na wimbile | Nzi kufia tuini si hasara |

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com

*Kuanzia swali la* **16** *mpaka* **30**, *jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Mtu anayefanya kazi ya kutafsiri makala kutoka lugha moja hadi nyingine ni
A. mkalimani.
B. mhariri.
C. mfasiri.
D. tarishi.

**17.** Neno '**mchango**' lina sauti ngapi?
A. Sita.
B. Tano.
C. Tatu.
D. Saba.

**18.** Msemo upi haujaambatanishwa vizuri na maana yake?
A. Piga msasa - fanya kuwa bora.
B. Enda chemba - kaa mahali faraghani.
C. Weka uporo - tenda jambo ovyoovyo.
D. Pika majungu - zuilia mafanikio.

**19.** Andika kinyume cha methali ifuatayo:
Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
A. Mtoto akilia wembe mpe.
B. Pilipili usiyoila yakuwashiani?
C. Mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina.
D. Dunia mti mkavu kiumbe usiuegemee.

**20.** Bainisha sentensi iliyo sahihi.
A. Huzuni mwingi ulitutanda alipotuacha mkono.
B. Mahali penginepo palitapakaa uchafu.
C. Karatasi hilo limechafuliwa na wino.
D. Nyasi iliyopandwa imekuwa refu.

**21.** Ainisha maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo:
Watoto wale **wote** wamefaulu mtihani **tena**.
A. kivumishi, kiunganishi.
B. kiwakilishi, kielezi.
C. kivumishi, kihusishi.
D. kivumishi, kielezi.

**22.** Badili sentensi ifuatayo katika usemi halisi.
Mwalimu alisema kuwa angetupa zoezi siku hiyo.
A. "Ningewapa zoezi siku hiyo."Mwalimu alituambia
B. "Nitawapa zoezi leo." Mwalimu aliwaambia.
C. "Nimewapa zoezi leo," Mwalimu alisema.
D. "Nitawapa zoezi leo," mwalimu alituambia.

**23.** Kiungo cha mwili kinachosafisha damu na kutoa mkojo ni
A. kibofu.
B. ini.
C. figo.
D. kongosho.

**24.** **Chungu** ni mdudu apendaye kula sukari. Chungu pia ni
A. aina ya kipele.
B. kitu kisichopendeza.
C. udongo anaotumia mifinyanzi.
D. ugonjwa wa majipu.

**25.** Kanusha:
Mgeni alipofika alimpata mwenyeji wake.
A. Mgeni hakufika wala kumpata mwenyeji wake.
B. Mgeni alipofika hakumpata mwenyeji wake.
C. Mgeni alifika ingawa hakumpata mwenyeji wake.
D. Mgeni asipofika huwa hampati mwenyeji wake.

**26.** Tambu sentensi yenye kiingizi kifaacho.
A. Po! Naumia, nisaidieni jamani!
B. Laiti! Ujanja wako umegunduliwa!
C. Hewala! Mambo hayo sitayashiriki!
D. Mashallah! Kijana yule ni mchezaji hodari!

**27.** Nomino **barua** na **simu** huorodheshwa katika ngeli gani?
A. LI - YA
B. U - ZI
C. I - I
D. I - ZI

**28.** Tegua kitendawili kifuatacho:
Mtama wangu hauhesabiki.
A. mawingu.   B. radi.
C. nyota.   D. mwezi.

**29.** Unda kitenzi kutokana na sifa **legevu**.
A. ulegevu   B. legea
C. mlegevu   D. ulegeaji

**30.** Ni sentensi ipi iliyotumia kiashiria cha mbali kabisa?
A. Maneno haya ninayokueleza yahifadhi moyoni.
B. Karibu na mti ule pana joka kubwa
C. Ndoo hizo alizozibeba zina maziwa
D. Nchi hii imeathiriwa sana na ufisadi

**Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com**

*Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali* **31 – 40**

Sanifu alikuwa mwalimu wangu wa somo la dini kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Alikuwa mwalimu mlezi wa darasa langu pia. Nilikutana naye katika siku yangu ya kwanza shuleni. Nuru ndiye aliyekuwa **akiwasajili** wanafunzi wa kidato cha kwanza. Mara tu aliponiona nikitembea kwa woga ubavuni pa baba yangu, aliondoka kutoka kitini pake na kutukaribisha. Uso wake ulivaa tabasamu iliyonikumbusha marehemu mama yangu ambaye alikuwa mwalimu pia. Bi sanifu alichunguza vyeti vyangu kuhakikisha kuwa havikuwa vimebatilishwa. Alipomaliza, aliandika jina langu katika orodha ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na kuniambia, "Karibu Tata. Mimi sasa nimekuwa mzazi wako".

Masomo yalikuwa mengi na magumu zaidi. Mitihani ilimhitaji mtu kutumia ujuzi wake kuyajibu maswali badala ya kuyakariri mawazo jinzi nilivyokuwa nimezoea. Ugumu wa masomo ulizidishwa na ugeni wangu katika mazingira ya mjini. Shule ya Nuru ilikuwa miongoni mwa shule chache za kisasa zilizojengwa katika mojawapo ya majiji nchini. Ilinibidi nijizoeshe kutumia vifaa vya kisasa kama vile 'misala ya ajabu' kama nilivyozoea kuiita. Haya yote yaliniwia vigumu mno. Ilibidi kila mara nimwendee Bi sanifu ambaye daima alinihimiza kutoenda nguu.

Ugeni uliniisha nikaanza kuingiliana na weledi wa mji. Wakanifunza njia za mkato za kufanya kazi za ziada shuleni. Almuradi kila mmoja alipania kuninoa kwa njia yake.

Bi Sanifu hakukoma kutambua mabadiliko katika hulka zangu. Sikuwa tena yule Tata mwenye haya ambaye miaka miwili iliyopita hakuweza hata kujitambulisha kwa mwalimu bila kutetemeka. Nilikuwa nimekomaa kiumri na kimatendo ila mawazo yangu yalikuwa yamekataa katakata kukomaa. Nilikuwa maji ambayo daima hufuata mkondo bila kujali.

Bi Sanifu aliniita ofisini mwake na kuniambia, "Tata, tangu nikutane nawe ulipokuja shuleni humu nimeshuhudia mabadiliko makubwa katika tabia yako. Umekuwa mwanafunzi mwenye adili za mchwa. Ingawa ulikuwa na matatizo mwanzoni, uliweza kuyakabili na kuinua alama zako. Isitoshe, umeweza kuwa na marafiki wengi humu shuleni. Hata hivyo, kuna jambo linalonitia wahaka kukuhusu. Tangu uingie katika kidato cha pili, marafiki zako wengi wamekuwa wanagenzi ambao wana miendo ya kutiliwa shaka. Baadhi yao **wameonyeshwa lango la shule** kwa visa mbalimbali kama vile utovu wa nidhamu darasani, matumizi mabaya ya dawa na mambo mengine ya ukiukaji wa sheria. "Wiki iliyopita, mwalimu wa zamu alikupata ukipiga domo na wenzio darasani. Isitoshe, umeanza mtindo wa kutofanya kazi ya ziada na kuyanakili majibu ya wenzako. Umekuwa mumunye ukaanza kuharibikia ukubwani".

Nilimtazama Bi Sanifu kwa muda, moyoni nikishangaa kwa nin anajihusisha na maisha yangu kiasi hicho. Nilianza kukumbuka maisha yangu ya awali; kifo cha mama, ujane wa baba wa miaka mitano na jinsi alivyojitahidi kutulea na kutuelekeza kwa kila jambo. Nilikumbuka msemo wa baba kuwa asiye na elimu hubakia kuwa mkunguni. Sasa mimi nilikuwa nimeanza kuchukua hatua za kwanza za safari hiyo. Naye Bi Sanifu alikuwa ameamua kuuwahi udongo ungali maji. Alinishauri kujiepusha na makundi ambayo yangeishia kulitumbukiza jina langu mashizi. Alinisihi kuyazingatia masomo yangu zaidi na kutumia muda wangu vyema ili kujikinga dhidi ya kuzorota kimasomo. Yeye, Bi Sanifu alikuwa amenitafutia udhamini kutoka kwa serikali. Karo yangu ingelipwa hadi kidato cha nne. Jukumu langu lilikuwa tu kujitahidi masomoni kadri ya uwezo wangu.

Mawaidha haya yalifungua ukurasa mpya maishani mwangu. Nilitanabahi kwamba nilikuwa na miaka miwili tu ya kuandaa mustakabali wangu. Nilijisuta kwa kutotumia muda wangu ilivyostahili. Nilikuwa nimezama katika kujionea huruma kwa kufiwa na mama na kusahau kuwa nilikuwa na jukumu la kuyadhibiti maisha yangu ipasavyo.

**31.** Neno **akiwasajili** lina maana gani kulingana na muktadha?

A. Akiwapokea.
B. Akiwakaribisha.
C. Akiwakagua.
D. Akiwaandikisha.

**32.** Chagua maelezo sahihi kulingana na aya ya kwanza.

A. Msimulizi aliyaogopa mazingira yake mapya.
B. Babaye msimulizi alifahamiana na Bi Sanifu.
C. Bi Sanifu alishuku kwamba vyeti vya msimulizi vilibatilishwa.
D. Baba hakuweza kuitambua hofu ya mwanawe.

**33.** Kwa nini Bi Sanifu alimkumbusha msimulizi kuhusu mama yake?

A. Kutokana na jinsi alivyotabasamu.
B. Alikuwa mwalimu kama mama yake.
C. Alisimama kuwakaribisha alipowaona.
D. Bi Sanifu alifanana sana na mama yake.

**34.** Chagua jawabu **lisilo** sahihi.

A. Changamoto huongezeka pale mtu asipozoeana na mazingira.
B. Ugumu wa masomo ulimfanya msimulizi kuchukia shule.
C. Mwandishi alizoea kuyakariri mawazo jinsi ilivyohitajika katika mtihani wa shule ya msingi.
D. Msimulizi hakuwa na ujuzi wa kutosha uliohitajika kujibu maswali katika shule ya upili.

**35.** Katika shule ya upili,

A. maisha ya Tata yalijaa shida tupu.
B. msimulizi alianza kupotoka mara moja.
C. mwandishi alijifunza mema na mawi.
D. Wanafunzi wengi walionyesha hulka ya utundu.

**36.** Aya ya nne inabainisha wazi kuwa,

A. wanafunzi wengine walimhimiza mwandishi afanye bidii.
B. Tata aliendelea kuwaogopa walimu wake.
C. Tata alikuwa sasa amefikia kuwa mtu mzima.
D. msimulizi hakuwa mwenye msimamo thabiti.

**37.** Maana ya **'wameonyeshwa lango la shule'** ni kuwa

A. wameyaasi masomo yao.
B. wamefukuzwa kutoka shuleni.
C. wamehimizwa kubadili mienendo.
D. miendo yao imeanza kutiliwa shaka.

**38.** Maasi aliyashiriki Tata shuleni ni pamoja na,

A. kupiga kelele darasani, kutokamilisha kazi.
B. kutumia mihadarati, kuungana na marafiki waovu.
C. wamehimizwa kubadili mienendo.
D. mienendo yao imeanza kutiliwa shaka.

**39.** Wazo linalojitokeza katika makala haya ni kuwa

A. msimulizi anashangazwa na hali ya Bi Sanifu kuyaingilia maisha yake.
B. kifo cha mama kilikuwa pigo lisilofutika katika maisha ya Tata na babaye.
C. kuyawazia sana matatizo ya nyuma kunaweza kudhoofisha utendaji.
D. kuungana na marafiki ni chanzo cha kupotoka kimaadili.

**40.** Chagua sifa za msimulizi kuhusiana na makala.

A. mwoga, anayejaribu kujibambua.
B. msamehevu, asiye na msimamo.
C. msikivu, mwenye kufuata rubaa.
D. mwonevu, asiyejali lolote.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41 – 50***

Sisi vijulanga tumepiga hatua kubwa kwenye vita dhidi ya ukongo wa Ukimwi. Si ajabu kwamba takwimu za hivi karibuni zinaonyesha maambukizi ya ugonjwa huu sasa yanaegemea kwa wakubwa. Ili kufanikisha hili, tumechukua hatua kadhaa.

Tumeunda vikundi vya kushauriana wenyewe kwa wenyewe. Kwenye vikundi hivi hatuoneani haya wala kujali kusemwa, tunayasema mambo vile yalivyo. Hili limetusaidia kujua mengi kuhusu ugonjwa huu. Isitoshe, mabango chungu nzima yamewekwa madarasani, maabarani na hata kwenye mabweni. Mabango haya yanabeba ujumbe mwingi kuhusu ugonjwa huu; kwa mfano, jinsi ya kujilinda mtu akipatikana na virusi. Mabango haya kwa jumla yanazidi kutuelimisha kuhusu ukongo huu.

Isitoshe, sisi tumeziacha mila zisizofaa kwa mfano, wasichana wamekataa kuozwa kwa wazee na pia kukeketwa. Wavulana nao wameasi **kuingia mava**. Aidha, shule zinatuitia washauri kutoka kwenye wizara husika au wanasaikolojia waje kutunasihi. Wametupatia ushauri ambao hata wazee huenda wasiwe nao.

Shuleni vilevile kuna idara ya ushauri kwa manafunzi ambazo zimetiliwa nguvu na serikali. Idara hizi hutoa ushauri kemkemu kwa wanafunzi kuhusu ugonjwa huu na mambo mengine mengi. Miziki mingine ambayo unaisikiliza imebeba ujumbe kuhusu uele huu pia. Imetushauri kwa mapana na marefu ili tuepuke maambukizi.

Tunaelewa fika kuhusu athari za kushiriki vyombo vyenye makali. Isitoshe, sio wengi wetu ambao wanauhitaji maana wengine videvu vyao ni vyeupe pe. Kadhalika kuna mashindano mengi sana kuhusu ugonjwa huu. Usisahau mijadala mingi ambayo tunakuwa nayo shuleni na hata kati yetu na shule nyingine. Tamasha za muziki pia zinatuwezesha kukariri mashairi mengi kuhusu ukimwi na kuimba nyimbo nyingi ambazo zina ujumbe huu.

Mitaala ya masomo pia imehusisha ugonjwa huu kwa mapana na marefu. Hivyo walimu wengi wana huduma ya kwanza. Hapa tunapata kuelezewa hatari za umajimaji au damu kutoka kwenye vidonda. Hivyo hatuvichezei na tunapompata mwenzetu akiwa na vidonda vilivyo wazi, humshauri aende kwa nesi akafungwe bendeji.

Aidha, hatulewi pombe ya kutulaza kwenye mitaro. Hivyo, uwezo wetu wa kufanya maamuzi haujaathirika sana. Isitoshe, hata hatuna fulusi nyingi na hivyo hatuwezi kumudu ulevi wa kupindukia. Vilevile, kinyume na wazee tunaelewa kuwa Ukimwi si kuchomekwa mizizi bali ni ukongo usio na tiba.

Hivyo wazee fuateni nyayo zetu. Msikubali uele huu uwafyeke. Eleweni kuwa tunawategemea sana kwa hivyo mchukue hatua. Mkifanya hivi mtauelewa na kujua namna ya kuuepuka. Pia, punguzeni matumizi ya pombe na ulevi wa aina yoyote ile.

Isitoshe, muache kuwa na macho ya nje maana hii ndiyo njia kuu ambayo kwayo ugonjwa huu huenea. Tafuteni wakati japo ni fupi msome magazeti na majarida yanayozungumzia ugonjwa huu. **Eleweni kuwa elimu ni bahari** na hakuna mtu anayeweza kuiogelea yote. Pia, mkipata nafasi hudhurieni mikutano, makongamano na warsha zinazoandaliwa kuhusu ugonjwa huu.

**41.** Chagua jibu lililo sahihi.
A. Maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi yamepungua.
B. Vijana sasa hawaathiriwi na ugonjwa wa Ukimwi.
C. Ugonjwa wa Ukimwi sasa unawaathiri wazee kuliko vijana.
D. Wazee kwa vijana wameweka mikakati ya kuepuka Ukimwi.

**42.** Vikundi vimewasaidia vijana kwa sababu,
A. wanaongezeana maarifa bila kufedheheka.
B. wanajifahamisha mengi kutoka kwa wazee.
C. wameweka mabango kila mahali shuleni.
D. wanafanya utafiti wa ugonjwa huu maabarani.

**43.** Wazo kuu katika **aya ya pili** ni kuwa,
A. penye urembo ndipo penye ulimbo.
B. elimu ni taa gizani huzagaa.
C. mkataa kikoa ni machawi.
D. elimu bila amali ni kama nta bila asali.

**44.** Baadhi ya mila zinazochangia kuenea kwa Ukimwi ni
A. upashaji tohara na ndoa.
B. kuingia mava na tohara ya vijana.
C. ukeketaji na ndoa.
D. kuwatahiri wasichana na kuridhi wajane.

**45.** Idara ya ushauri kwa wanafunzi,
A. ilibuniwa na serikali kutoa nasaha kuhusu Ukimwi.
B. inadhibitiwa na serikali ili kuwatetea vijana.
C. inayaangazia masuala ya vijana kwa mapana na marefu.
D. ni njia kuu ya kudhibiti matatizo yote shuleni.

**46.** Taja njia za kukabiliana na Ukimwi zilizoangaziwa katika **aya ya tano.**
A. Mijadala na tamasha za muziki.
B. mashindano ya michezo na kughani mashairi.
C. kutotumia vyombo vyenye makali na kualika washauri.
D. michezo ya kuigiza na kughani mashairi.

**47.** Mitaala ya elimu imewafaa vipi vijana?
A. Imefanya elimu ya Ukimwi kuwa somo la lazima.
B. Imeimarisha mafunzo ya huduma ya kwanza.
C. Imewashurutisha walimu wote kufunza kuhusu Ukimwi.
D. Imeliwezesha suala husika kushughulikiwa kitaaluma.

**48.** Si kweli kusema kuwa,
A. uhaba wa fulusi unadhibiti nyendo za vijana.
B. vijana hawa hawalewi asilani.
C. waunguzi shuleni wanasaidia kukabiliana na maambukizi.
D. vijana kwenye makala wana maarifa zaidi ya wazee.

**49.** Makosa ambayo yamehusishwa na wazee kwenye makala haya ni,
A. ulevi wa kupindukia na kukosa uaminifu katika ndoa.
B. kulewa kupindukia na kutoshauri vijana.
C. ukosefu wa maarifa na macho ya nje.
D. kuwapuuza vijana na kulewa kupita kiasi.

**50.** **'Eleweni kuwa elimu ni bahari'** Hii ni sitiari yenye maana kuwa, elimu
A. ina manufaa mengi.
B. hupatikana kotekote.
C. haina mwisho.
D. ni ya aina nyingi.

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com